

Original Research Article

Ubainishaji wa Maswali ya Balagha kwa Kuzingatia Viashiria vyakimofolojia katika Mazungumzo ya Kiswahili

Sikitu Elias^{1*}, Prof. Pendo Salu Malangwa², Dkt. Musa Mohamed Shembilu(PhD)³

¹PhD Student in Swahili, Department of Swahili Language and Linguistics, Institute of Swahili Studies, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania

²Research Supervisor, Associate Professor, Department of Swahili Language and Linguistics, Institute of Swahili Studies, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania

³Research Supervisor, Lecturer and Head of the Department of Swahili Language and Linguistics, Institute of Swahili Studies, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania

Article History

Received: 11.04.2025

Accepted: 17.05.2025

Published: 23.05.2025

Journal homepage:

<https://www.easpublisher.com>

Quick Response Code



Abstract: Makala hii inahu ubainishaji wa maswali ya balagha kwa kuzingatia viashiria vyakimofolojia katika mazungumzo ya Kiswahili. Maswali ya balagha ni maswali yasiyohitaji majibu yenyelengo la kufikisha ujumbe kwa wahusika. Maswali haya hutumika kama mbadala wa kauli mbalimbali. Ili kupata kile kilichokusudiwa, maswali haya hayana budi kubainishwa. Suala la ubainishaji wa maswali ya balagha hutofautiana kulingana na lugha. Kwa kuwa suala la ubainishaji wa maswali ya balagha katika Kiswahili haliko bayana, makala hii inalenga kutoa maarifa hayo kwa kuonesha viashiria vyakimofolojia vinavyotumika kubainisha maswali ya balagha katika mazungumzo ya Kiswahili. Data za Makala hii zilipatikana kutoka katika mazungumzo ya kwenye vibanda vya mpira, mamantilie na vijiwe vya bodaboda kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Mbeya. Mbinu ya ushuhudiaji wa kushiriki ilitumika kukusanya data. Aidha, uchambuzi wa data umefanywa kwa kutumia mkabala wa maelezo. Nadharia ya Tendo-uneni ya Searle (1979) imetumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za Makala hii. Matokeo yanaonesha kuwa katika mazungumzo ya Kiswahili, maswali ya balagha huweza kuashiriwa na viashiria vyakimofolojia. Kuna viashiria kama vialami pragmatiki, viunganishi na vitenzi ambavyo huukilia fasiri ya kibalagha. Makala hii inabainisha kuwa pamoja na kwamba kuna viashiria vyakimofolojia, bado muktadha wa mazungumzo ndio unaovifanya vipate nguvu ya kubainisha maswali ya balagha. Makala hii inapendekeza tafiti nyingine zifanyike katika miktadha tofautitofauti ili kuendelea kuweka bayana suala la ubainishaji wa maswali ya balagha katika Kiswahili kwa ajili ya kujenga maarifa ya kisemantiki na kipragmatiki.

Keywords: Maswali ya balagha, mazungumzo, viashiria, ubainishaji, kimofolojia, Kiswahili.

Copyright © 2025 The Author(s): This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution 4.0 International License (CC BY-NC 4.0) which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

1.0 UTANGULIZI

Uulizaji wa maswali ni njia mojawapo ya kuendeleza mazungumzo. Kwa kuwa swali ni nyenzo ya kutafutia taarifa asizozifahamu muulizaji (Lakoff, 1973), msikilizaji hutakiwa kutoa majibu ya kile alichouliwiza ili taarifa hizo ziweze kusatikana. Fiengo (2007) anaeleza kuwa tunapouliza maswali tunakuwa tunatamka sentensi ambazo hazijakamilika kitaarifa kwa namna moja au nyingine. Kutokamilika kwa taarifa hizo kunahusiana na upungufu tulionao au kile tulichokosa. Ilgizovna (2018) anatumia sentensi ulizi kumaanisha swali na kueleza kuwa sentensi ulizi ni mbinu ya lugha

ambayo hulenga kutafuta taarifa kwa kuhitaji majibu kutoka kwa wasikilizaji.

Pamoja na kwamba maswali hulenga kupata taarifa au ufanuzi kutoka kwa wasikilizaji, si wakati wote maswali yanayoulizwa hulenga kupata taarifa au ufanuzi zaidi. Wakati mwengine, wazungumzaji huuliza maswali yenyelengo makusudio mengine (Athanasiadou, 1990; Frank, 1990; Wang, 2014). Katika makala hii, maswali yenyelengo makusudio mengine na yasiyohitaji majibu kutoka kwa wasikilizaji yanajulikana kama maswali ya balagha. Ilie (1994) anaeleza kuwa maswali ya balagha hufanya kazi kama swali na kama

*Corresponding Author: Sikitu Elias

PhD Student in Swahili, Department of Swahili Language and Linguistics, Institute of Swahili Studies, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam, Tanzania

kauli. Kwa mujibu wa Searle (1979), maswali kama haya ni matendo-uneni yasiyowazi kwa kuwa hutekeleza matendo-uneni mengine kwa namna isiyo wazi. Sakamoto (2018) anafafanua zaidi kuwa maswali ya balagha huleta utata katika kuyafasiri kutokana na matumizi ya namna mbili, yaani, kutaka taarifa pamoja na kuwa na dhima za kibalagha. Hivyo, ili wasikilizaji waweze kumaizi kilichokusudiwa na muulizaji hawana budi kuyabainisha.

Kumekuwepo na mjadala kuhusu ubainishaji wa maswali ya balagha. Wapo wanaosema kuwa maswali ya balagha hubainishwa kuititia muktadha wa matumizi yake tu na wengine wanaosema kuwa kuna viashiria vya kiisimu ambavyo husaidia katika ubainishaji wa maswali ya balagha. Wataalamu kama Schmidt-Radefeldt (1977), Sakamoto (2018), Dehé na Braun (2019) wanathibitisha kuwa maswali ya balagha na maswali ya kawaida hutofautiana kuititia viashiria mbalimbali, ambavyo hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Kwa maneno mengine kila lugha ina namna yake ya ubainishaji wa maswali ya balagha. Mathalani, Schmidt- Radefeldt (1977) na Sakamoto (2018) wanaeleza kwamba viro viashiria vya kiisimu na kimuktadha vinavyoweza kubainisha maswali ya balagha. Kwa mfano, katika lugha kama Kijapani, maswali ya balagha huundwa na vipashio fulani mwishoni mwa sentensi, ambapo vipashio hivyo ndivyo vinavyoweza kuukilia dhima husika.

Sadock (1971; 1974) anaeleza kuwa katika lugha ya Kiingereza, kuna vipashio fulani ambavyo huambatana na maswali ya balagha na sio maswali ya kawaida. Anabainisha vipashio kama *after all, yet, by any chance* na kusema kuwa vipashio hivi hutokeea katika maswali ya balagha na sio katika maswali ya kawaida. Pia, anataja sifa nyingine za maswali ya balagha kuwa ni kufuati na kishazi cha *yet*, sifa ambayo haipo katika maswali mengine ya kawaida. Han (2002) naye anashikilia msimamo kuwa maswali ya kawaida na maswali ya balagha hayafanani bali hutofautiana. Anaeleza kuwa, maswali haya hata kumuundo hayako sawa. Kwa mfano; anaeleza kuwa katika lugha ya Kiitaliano, maswali yenye uelekeo hasi na chanya huwa na vipashio fulani ambavyo hufanya maswali hayo yaeleweke kama maswali ya balagha. Anaonesha mfano wa vipashio kama *any, ever, stil, yet* kwamba hupatikana hata katika maswali ya kawaida lakini vipashio kama *lift a finger, budge an inch, until, at all, a bit* hupatikana katika maswali ya balagha pekee. Mawazo ya mtaalamu huyu yanaonesha wazi kuwa katika lugha ya Kiitaliano, maswali ya balagha huwa na vipashio fulani maalumu ambavyo huweza kuyafanya yabainishwe.

Kwa upande wao Bhattachari, Cytryn, Feldman na Park (2015) walichunguza maswali ya balagha kwa kutumia program ya *n-gram*. Katika uchunguzi wao walibaini kuwa maswali ya balagha huweza

kupambanuliwa kutoka katika maswali mengine ya kawaida kileksika, kisintaksia na kimuktadha. Wanataja vibainishi vya maswali ya balagha kama vile uchaguzi wa maneno katika swali ambao husaidia kujua lengo la mzungumzaji. Wanaeleza kuwa kuna maneno kama vile *well, you know* ambayo ni vibainishi vya wazi vya maswali ya balagha. Pia, viashiria vya ukarusha kama vile *budge an inch, give a damn, lift a finger*, vitenzi visaidizi kama vile *could, would* na maelezo mengine kama *yet* na *after all* huweza kubainisha maswali ya balagha.

Aidha, Sakamoto (2018), alifanya uchunguzi linganishi wa viashiria vya ubalagha katika lugha ya Kiingereza na Kijapani. Anaeleza kuwa maswali ya balagha hubainishwa kuititia vipashio tamati vinayowekwa mwishoni mwa swali. Anaongeza kwa kusema kuwa Kijapani kina utajiri mkubwa wa viambishi tamati ambavyo husaidia kubainisha aina ya sentensi husika. Anatoa mfano katika lugha ya Kijapani kuwa kipashio *to yuu no kinapowekwa* mwishoni mwa sentensi ulizi, moja kwa moja huashiria ubalagha. Maelezo ya Sakamoto (2018) yanaelekeana na yale ya Jeong (2018) anayeeleza kuwa katika lugha ya Kikorea, viambishi tamati vinavyotokea mwishoni mwa sentensi ulizi huwa na dhima za kibalagha. Anatoa mfano wa viambishi *-nya* na *-ni* kuwa hutumika kuunda maswali ya balagha yanayoelezea hisia na kudokeza kutokukubaliana na jambo fulani. Matokeo ya utafiti uliofanywa na Sakamoto (2018) na Jeong (2018) yanadhihirisha kuwa ubainishaji wa maswali ya balagha hutofautiana baina ya lugha moja na nyingine na kwamba kila lugha ina upekee wake katika kubainisha maswali ya balagha.

Halikadhalika, Wang (2021) anaeleza kuwa katika lugha ya Kimandarin [¹], kuna vipashio ambavyo vikionekana katika maswali, moja kwa moja huashiria ubalagha wa maswali husika. Anaendelea kufafanua kuwa hii inatokana na kwamba vipashio hivyo vinapowekwa katika maswali mara nyingi hufanya maswali hayo kipragmatiki yawe na sifa ya maswali ya balagha kama kuwa na uelekeo hasi na kutohitaji majibu. Wang (2021) anabainisha kuwa maswali ya balagha yenye muundo wa *bushi...ma* huwa na dhima ya kuonesha matendo pingamizi kama vile kupinga hoja tangulizi ya mzungumzaji, kumkumbusha msikilizaji kile kilichotafsiriwa tofauti na kujitetea pale anapokosolewa. Anaendelea kueleza kuwa matendo pingamizi kama kulaumu, kupinga hoja tangulizi na kushushua yanayoukiliwa na *bushi...ma* mara nyingi hupatikana katika maswali ya balagha na maswali kanushi kwa ujumla na sio katika maswali ya kawaida.

Kwa ujumla mawazo ya wataalamu waliopitiwa kuhusu ubainishaji wa maswali ya balagha yana mchango katika makala hii kwa kuwa yanatoa mwanga kuhusiana na ubainishaji wa maswali ya balagha.

¹ Kimandarin ni Kichina sanifu.

Wataalamu hao wanathibitisha kuwa maswali ya balagha yanaweza kubainishwa kupitia viashiria vya kiisimu vikiwemo na viashiria vya kimofolojia. Pamoja na ufaafu wa mawazo hayo, bado katika lugha ya Kiswahili kunakosekana maarifa ya namna maswali ya balagha yanavyobainishwa. Hali hii inafanya tushindwe kuegemea matokeo ya tafiti zao kwa kuwa kila lugha ina namna yake ya ubainishaji wa maswali ya balagha. Hivyo, Makala hii inaweka bayana jambo hili kwa kuonesha viashiria vya kimofolojia vinavyotumika kubainishwa maswali ya balagha katika mazungumzo ya Kiswahili.

2.0 Nadharia

Makala hii imetumia Nadharia ya Tendo-Uneni (NTU) ya Searle (1979). Nadharia hii iliasisiwa na John Austin (1962) katika kitabu chake cha *How to Do Things with Words*. Baadaye ikaendelezwa na Searle (1969; 1979). Austin (1962) anaeleza kuwa si mara zote lugha hutumika kufafanua mambo bali hutumika kutenda na anayaita matamko kama haya kuwa ni matendo-uneni. Kupitia usemi mtu anaweza kutoa amri, kutoa taarifa, kushangaa, kuomba msamaha, kusifia, kukejeli au kuuliza swalii. Pia, Austin anagawa usemi katika aina mbili, yaani, usemi thabiti na usemi tendeshi. Kwa mtazamo wake, usemi thabiti ni usemi ambao hauhusishi matendo, yaani, ni kauli yenye kutathminiwa kwa masharti-ukweli, lakini usemi tendeshi ni usemi unaohusisha matendo, yaani, kwa kutamkwa kwake tu kuna athari inayotokea katika ulimwengu halisi. Hata hivyo, mtaalamu huyu alijikita katika kujadili usemi tendeshi na kwamba usemi huu unapotolewa huhusisha mabadiliko katika ulimwengu halisi, yaani, matendo-uneni. Mawazo haya yaliboreshwaa na wataalamu kama vile Searle (1969; 1979), Graham (1977), Bach na Harnish (1979), Birner (2013), ambao wanaelekeana katika maelezo yao kuwa katika matendo-uneni, kuna yale yenye vitenzi tendeshi vya wazi na matendo-uneni yasiyo na vitenzi tendeshi vya wazi. Searle (1979) aliboresha zaidi kipengele hiki kwa kuweka bayana kuwa mzungumzaji anaweza kutamka sentensi kumaanisha kile atamkacho lakini akawa na maana nyingine zaidi. Anaendelea kueleza kuwa matendo-uneni ya namna hii ni matendo-uneni yasiyo wazi kwa kuwa tendo-uneni moja hutumika kutenda tendo-uneni jingine kwa namna isiyowazi. Msingi huu umekuwa faafu kwa makala hii kwa kuwa maswali ya balagha ni mionganoni mwa matendo-uneni yasiyo wazi kwani muundo wake kama swalii haufanyi kazi ya kuhitaji majibu kama kawaada ya maswali.

Searle (1979) anaeleza kuwa maana ya matendo-uneni yasiyo wazi hupatikana kwa kuzingatia hali ya utoaji usemi husika, maandalizi ya kutoa usemi, viambajengo (vigambe husika) na ukweli uliopo. Pia, anaongeza kuwa katika matendo-uneni yasiyo wazi,


mzungumzaji anatamka na kumaanisha zaidi ya alichosema kwa kuegemea katika usuli wa pamoja wa taarifa, taarifa za kiisimu na zisizo za kiisimu (kimuktadha), urazini (uwezo wa utambuzi) pamoja na mahitimisho yanayofanywa na msikilizaji. Pia, Searle (1979) anaeleza kuwa tendo-uneni lisilowazi haliwezi kuwa fiche kwa asilimia zote. Mzungumzaji anapotoa usemi wake hutumia viashiria fulani ambavyo husaidia kubaini tendo-uneni husika. Mawazo haya yanabainika pia kwa wataalamu walioendezea nadharia hii kama vile Sadock (1971/1974) ambapo walidhihirisha kuwa matendo-uneni yasiyo wazi hayawi fiche moja kwa moja bali huhusisha baadhi ya viashiria vya tendo-uneni husika katika muundo wa nje wa usemi. Msingi huu ya umesaidia katika uchambuzi wa data za makala hii kwa kuwa maswali ya balagha yalibainishwa kwa kuzingatia vipashio mbalimbali vya kimofolojia ambavyo vinapatikana katika muundo wa swalii. Kuwepo kwa viashiria vya kimofolojia kulifanya maswali yatambulike kama maswali ya balagha kutokana na ujumbe ulioeleweka.

3.0 METHODOLOJIA

Data za Makala hii zilipatikana kupitia mbinu ya ushuhudiaji wa kushiriki wa mazungumzo ya kwenye vibanda vya mpira, mamantilie na vijiwe vya bodaboda vinavyopatikana katika kata ya Buguruni, Wilaya ya Ilala katika Mkoa wa Dar es Salaam na kata ya Ruanda, Wilaya ya Mbeya Mjini katika Mkoa wa Mbeya. Mazungumzo yalirekodiwa kwa njia ya kinasasauti na data nyingine zilirekodiwa kwenye shajara huku itikeli ikizingatiwa. Baadaye, mazungumzo hayo yalinukuliwa kwa kutumia mfumo wa alama za unukuzi wa Jefferson (2004) na kisha kuchanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na mbinu ya uchanganuzi kilongo.

4.0 Ubainishaji wa Maswali ya Balagha kwa Kuzingatia Viashiria vya Kimofolojia katika Mazungumzo ya Kiswahili

Viashiria vya kimofolojia ni maumbo mbalimbali ya maneno yanayodhihirika katika maswali. Maneno hayo yanapodhihirika katika maswali, hufanya maswali husika yafasiriwe kama maswali ya balagha. Hali hii husababisha maswali husika yapoteze sifa ya kuhitaji majibu au taarifa kutoka kwa wasikilizaji. Katika Makala hii, jumla ya maswali ya balagha mia sita na ishirini na sita (626) yalichambuliwa ambapo maswali ya balagha mia moja na kumi (110), sawa na asilimia arobaini na nne nukta mbili (44.2%), ya maswali ya balagha yalibainishwa kupitia viashiria vya kimofolojia. Maswali ya balagha yalidhihirika kupitia viashiiria vya kimofolojia kama vile vialami pragmatiki kwa asilimia arobaini na saba (47%), viunganishi kwa asilimia kumi na tatu (13%), na vitenzi kwa asilimia arobaini (40%) kama inavyooneshwa katika kielelezo Na. 4.1



Kielelezo Na. 4.1: Idadi ya Maswali ya Balagha Yaliyobainishwa kwa Kuzingatia Viashiria vyta Kimofolojia
Chanzo: Data za Uwandani (2022)

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha idadi ya maswali ya balagha kwa kila kiashiria cha kimofolojia. Kupitia takwimu hizi, vialami pragmatiki vinaonekana kuwa na nafasi kubwa ya kuashiria ubalagha wa maswali vikifatiwa na vitenzi kisha viunganishi. Ufanuzi zaidi wa viashiria hivi unatolewa katika sehemu inayofuata.

4.1 Vialami Pragmatiki

Vialami pragmatiki ni maneno au virai kutoka katika kategoria mbalimbali za kisintaksia kama vile vielezi, viunganishi, vitenzi, vihisishi na virai vihusishi (Kibiki, 2020). Makala hii inabainisha kuwa vialami pragmatiki vinapotumiwa katika maswali, hufanya maswali husika kupata fasiri ya kibalagha. Aidha, vialami pragmatiki husaidia kujenga mazungumzo yanayoendelea kwa kuhusisha usemi tangulizi au usemi fuatizi. Mfano, katika data ifuatayo kialami pragmatiki kilichotumika kuunda swalii kimefanya swalii hilo lipoteze sifa ya kuhitaji taarifa kwa kuwa mzungumzaji anatoa ujumbe na si kutaka jibu kutoka kwa msikilizaji.

Data Na. 1:

1. A. ... Ni nani aliye kwenda kumwona?
2. B. Watu kibao wameenda, umebaki wewe tu.
3. A. Umejuaje kama sijaenda?
4. B. A::h! Ulienda lini?↓(anauliza huku akisindikiza swalii lake na ishara za uso)).
5. A. Sasa kwani kwenda kumwona mtu lazima nifanye matangazo?
6. B. Ungeenda ingejulikana tu *bro!*
7. B. Sio lazima ijulikane na ndio maana hujui kama nimeenda au la. Kwa hiyo, usinibishie.

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha bodaboda, Mbeya (2022).

Kinachobainika katika data hii ni kwamba mzungumzaji A na mzungumzaji B wanabishana kuhusu kwenda kumwona mwenzao aliye patwa na matatizo. Katika muktadha huo inaonesha wazi kuwa mzungumzaji A hakwenda kumwona mwenzao ingawa

anauliza endapo wengine walikwenda. Kutokana na mazingira yalivyokuwa kwa vyovytile mzungumzaji B anatambua wazi kuwa mzungumzaji A asingeweza kwenda. Mzungumzaji B anauliza swalii huku akitumia kialami pragmatiki “aaah!” na kukitamka kwa kuvuta irabu “a” na swalii kuishia na kiimbo cha kushuka. Kupitia matumizi ya kialami pragmatiki, moja kwa moja swalii linapoteza sifa ya kuhitaji majibu na hivyo linabeba ujumbe wa kubeba ndani yake. Hii inajidhihirisha katika majibu ya mzungumzaji A katika zamu ya 5 “Sasa kwani kwenda kumwona mtu lazima nifanye matangazo?” Ingawa, jibu hili limekaa katika muundo wa swalii linaonesha kwamba mzungumzaji A anapinga kitendo cha kubewa na kwamba anayembeza huenda hajui kwani si lazima kufanya matangazo ili kila mmoja ajue. Pia, mzungumzaji A hajatoa jibu la wakati aliokwenda bali anaonesha kuwa ameelewa ujumbe uliowasilishwa kupitia swalii kuwa anabewza ndipo naye anaamua kutumia swalii kama jibu kukanusha ujumbe wa swalii B. Hivyo, utambuzi wa dhima ya swalii hili unaukiliwa na matumizi ya kialami pragmatiki *aaah*.

Mfano mwingine wa matumizi ya kialami pragmatiki kilichobainika katika utafiti huu ni neno “kweli”. Utafiti huu umebaini kuwa katika mazingira fulani ya mazungumzo ya Kiswahili, neno “kweli” linapotumika kuunda swalii basi swalii husika hufasiriwa kama swalii la balagha. Data ifuatayo inadhihirisha hili:

Data Na. 2:

1. A. Kweli wewe ndio wa kunifanyia hivi?
2. B. Hapana dada unajua wazi kuwa siwezi kukufanya hivyo (0.2) hao wamekudanganya.
- A. Wanidanganyi kwa maslahi gani wakati wewe ndiye uliyekwenda kule hiyo juzi?
3. B. Unajua dada hata njiezeleze vipi hutanielewa ila kuna siku utajua ukweli wote.
4. A. Sasa wewe unataka usielezwe ukweli? Kujieleza huko vipi?

Chanzo: Mazungumzo katika kibanda cha mamantilie, Mbeya (2022).

Data Na. 5 zamu ya 1, inaonesha matumizi ya neno “kweli” katika swali. Katika uulizaji wa swali unaoambatana na matumizi ya neno “kweli”, ilibainika kuwa msikilizaji amepata fasiri ya kibalagha ambayo ni lawama badala ya kuchukulia kuwa swali linahitaji kupatiwa majibu. Utafiti huu umebaini kuwa swali lenye kuambatana na kipashio “kweli” huulizwa katika mazingira ya kulaumu huku mzungumzaji akistaajabia matendo aliyofanyiwa kana kwamba yasingewenza kufanywa na mhusika. Muulizaji anaposema “kweli wewe ndio wa kunifanyia hivi?” Anamaanisha kuwa “wewe sio wa kunifanyia hivi, yaani, hukustahili kunifanya hivi”. Katika swali hili muulizaji hakusudii kupata jibu la ndiyo au hapana bali analenga kumlaumu mhusika kwa kitendo alichomfanyia jambo ambalo linafanya swali husika lisiwe swali la kawaida. Pia, katika utafiti huu imebainika kuwa kipashio “kweli” kina nguvu ya kuashiria ubalagha kiasi kwamba kikiondolewa, basi swali linaweza kupoteza sifa ya ubalagha na kueleweka kama swali la kawaida.

4.2 Viunganishi

Viunganishi ni aina ya maneno ambayo hutumika kuunganisha dhana au sentensi zaidi ya moja. Aidha, katika utafiti huu, kuna maswali ya balagha ambayo yilibainishwa kupitia viunganishi. Matumizi ya viunganishi kama “hata hivyo”, “lakini”, na “hata” yalionekana kuukilia maana ya kibalagha katika swali kwani kuwepo kwake kunaliondolea swali sifa ya kuhitaji taarifa. Data ifuatayo inaonesha namna neno “hata hivyo” liliyotumika katika swali:

Data Na. 3:

1. A. Ah! Sitarudia tena ule upuuzi nakwambia, yaani, *buku jero* ndio iniponze!
2. B. Hata hivyo nani alikutuma uende? Unajua mambo mengine ni kujitakia, we ulivyoona wenzio tunasita ulishindwa kujiongeza?
3. A. Si unajua tena mtu ukiwaza hesabu *bro*? Unajikuta huwezi kuacha hela ipite. Aisee! Ila kule ni mbali halafu barabara ni mbovu sijapata kuona, unajua nilikuwa sijapita njia ile muda mrefu.

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha bodaboda, Mbeya (2022).

Katika muktadha huu mzungumzaji A anaonesha kujutia kwa jambo alilolifanya la kumsafirisha abiria kwa nauli ndogo wakati aendako ni mbali na barabara sio nzuri. Katika zamu ya 2 mzungumzaji B anamuuliza swali ambalo kutoptana na neno “hata hivyo” lililotumika kuunda swali hilo, kunafanya fasiri ya kibalagha ichukue nafasi. Msikilizaji A anagundua kuwa muulizaji B, hakusudii jibu bali analenga kumkosoa kwa kuwa alipoona wenzake hawataki kwenda yecheakaamua kwenda bila kufikiri kwa nini wenzake hawataki kwenda. Kinachoonesha

kuwa mzungumzaji A amekosolewa na mzungumzaji B ni matumizi ya neno “hata hivyo” katika swali na majibu ya msikilizaji, yaani, mzungumzaji B yanaonesha kuwa swali liloulizwa ni swali la balagha.

Pia, matumizi ya kiunganishi “hata” katika swali yanachochea fasiri ya kibalagha iweze kupatikana kuliko kujua kuwa swali linahitaji taarifa fulani. Data ifuatayo inadhihirisha hili:

Data Na. 4:

1. A. ((Anaingia bosi anakuta binti mmoja anafanya kazi ya kuchambua mboga huku mwanae akiwa amekaa tu bila kufanya chochote ndipo anamua kuuliza swali)) Hivi huwezi hata kumsaidia mwenzako?
2. B. ((Anainuka kimya kimya na kwenda kumsaidia)).

Chanzo: Mazungumzo katika kibanda cha mamantilie, Dar es Salaam (2022).

Katika muktadha wa mazungumzo haya inaonesha kuwa mzungumzaji A amekerwa na tabia ya mwanae kukaa bila kumsaidia mwenzake. Anatumia swali la balagha kama njia ya kumkosoa na si kuhitaji jibu. Matumizi ya neno “hata” katika swali yanaondoa sifa ya swali kutaka jibu kwani msikilizaji anapata fasiri ya kibalagha kwa kuelewa dhima iliyobebwa katika swali hilo. Kama swali hilo lisingekuwa na neno “hata” ni rahisi kueleweka kama swali la kawaida lakini matumizi ya neno “hata” yanaoliondolea swali husika nguvuya kueleweka kama linahitaji majibu.

4.3 Vitenzi

Kipashio kingine cha kimofolojia kinachowezza kuashiria maswali ya balagha ni vitenzi. Katika utafiti huu kuna maswali ya balagha yalidhihirishwa kupitia matumizi ya vitenzi vya kiutambuzi kama “fikiri”, “dhani”, “hisii” na “taka”. Ilabainika kuwa vitenzi vya namna hii vinapotumiwa kuunda swali hutoa nafasi ya swali husika kupata fasili ya kibalagha kuliko kuhitaji majibu au taarifa kutoka kwa msikilizaji. Data ifuatayo inadhihirisha hili:

Data Na. 5:

1. Ninataka niende nikachukue mchele kwa ((anataja jina))
2. Ahaa! Basi unaweza ukapitia na kale kamzigo kangu!
3. Unasema kamzigo? Hivi unafikiri ule mzigo ni mdogo?
4. Sasa una ukubwa gani? Ningekuwa sina kazi ningeufuata mwenyewe.
5. Kwa hiyo, unataka kusema ule mzigo ni mdogo? Mimi nilikuwa nakutahadharisha tu usiseme kamzigo kana kwamba ni rahisi kuubeba.

Chanzo: Mazungumzo katika kibanda cha mamantilie, Mbeya, (2022).

Data Na. 4 inaonesha matumizi ya kitenzi “fikiri” katika swali yanavyoukilia fasiri ya kibalagha.

Matumizi ya kitenzi “unafikiri” katika swali liloulizwa na mzungumzaji A katika zamu ya 3, yanafanya swali hilo lipoteze sifa ya kuhitaji majibu ya ndiyo au hapana. Kuwepo kwa kitenzi hicho kunafanya swali liukilie fasiri ya kibalagha kuliko kuhitaji majibu. Hicho, mzungumzaji A anaposema “hivi unafikiri ule ni mzigo mdogo?” analenga kumkosoa mzungumzaji B kwa kauli yake na kwamba ule si mzigo mdogo bali ni mkubwa na hivyo itakuwa vigumu kuuchukua. Pia, kupitia swali hilo, mzungumzaji A analenga kukataa ombi la mzungumzaji B kwa namna isiyowazi. Katika muktadha wa mazungumzo hayo inadhihirisha kuwa mzungumzaji B alielewa kuwa anapingwa kwani anauliza swali linalopinga mtazamo wa mzungumzaji A pale anaposema “sasa una ukubwa gani?”. Mzungumzaji A anapouliwa swali hili, anakusudia kupinga mtazamo wa mzungumzaji B ambaye ameonesha kumkosoa kwa kauli yake ya kusema “kale kamzigo” ilhali mzigo ni mkubwa. Hivyo, matumizi ya kitenzi “unafikiri” katika swali husika ndiyo yaliyochoechea fasiri ya ubalagha kupatikana.

Pia, mfano mwengine ni matumizi ya kitenzi cha kiutambuzi “dhani”. Kitenzi hiki hakitofautiani na kitenzi fikiri ambapo matumizi yake katika swali, yanafanya fasili ya kibalagha iweze kupatikana. Katika data hiyo, matumizi ya kitenzi “dhani”, moja kwa moja kulifanya swali lieleweke kuwa linakusudia kukosoa kitendo au usemi tangulizi na kwamba kupitia swali husika, msikilizaji anapata majibu kanushi kuliko majibu chanya. Data ifuatayo inadhihirisha hili:

Data Na. 6:

1. ((Mmiliki wa biashara anaingia na kuanza kuuliza)) Hivi umeshapaki ugali? Maana naona kama umeanza kazi nyingine.
2. Hapana, nimejisahau nilikuwa nawapakulia wateja chakula.
3. Mpaka sasa? Ugali ukipoa unadhani nani atakayekula kipolo?
4. Ngoja nimalizie hapa naenda kuupaki.

Chanzo: Mazungumzo katika kibanda cha mamantilie, Mbeya (2022).

Data Na. 6 katika zamu ya 3, inaonesha matumizi ya kitenzi “dhani” katika swali yanavyolifanya swali husika lipate fasiri ya kibalagha zaidi ya kujua kuwa linahitaji majibu. Katika swali “unadhani nani atakula kipolo?”, inamaanisha kuwa hakuna atakayekula kipolo. Hivyo, badala ya kutaja mtu au watu watakaokula kipolo anaamua kujitetea na kuahidi kwenda kutekeleza kitendo cha kupakia ugali kwa kuwa anaelewa kwamba swali halihitaji majibu.

Vilevile, matumizi mengine ni ya kitenzi “taka”. Makala hii inaonesha kuwa kitenzi hiki kinapotumiwa katika swali kunachoechea fasiri ya kibalagha kupatikana kuliko kuonesha kuwa swali linahitaji majibu au taarifa kutoka kwa msikilizaji.

Data Na. 7:

1. A. Umeona lakini kwamba kagusa ule mpira?
2. B. Angegusa refa angeona.
3. A. Hakuna! Hapo kuna jambo, unataka kuniambia refa hajaona ule mkono kweli?
4. B. Kwa hiyo, wewe ni refa? Nenda basi kachezeshe.

Chanzo: Mazungumzo katika kibanda cha mpira, Dar es Salaam (2022).

Katika data Na. 7, swali la mzungumzaji A katika zamu ya 3 ni swali la balagha yaani halihitaji majibu bali linawasilisha ujumbe wa kupinga hoja ya mzungumzaji B uliotolewa katika zamu ya 2. Matumizi ya kitenzi “taka” katika swali husika yanafanya fasiri ya kibalagha ipatikane kuliko kuonesha kuwa swali linahitaji majibu au taarifa kutoka kwa msikilizaji. Neno “taka” katika swali hilo linaukiria hali ya kutokubaliana. Hivyo, kinachoelewka hapo ni kwamba mzungumzaji A anapinga hoja ya mzungumzaji B. Pia, kudhihirisha hili, mzungumzaji B katika zamu ya 4 anaonesha kuwa ameellewa nia ya mzungumzaji A ndio maana naye anauliza swali lenye nia ya kuteteta hoja yake.

Aidha, Makala hii inadhihirisha kuwa vitenzi vyta uwezo mathalani, “weza” vinapounda maswali hufanya maswali husika kuwa na sifa ya maswali ya balagha. Imebainika kuwa maswali yanayotumia kitenzi “weza” mara nyingi yanaashiria dhima ya kuomba kuliko kutaka kujua uwezo alionao msikilizaji kuhusiana na kitendo husika. Data ifuatayo inadhihirisha hili:

Data Na. 8:

1. A. Hivi unaweza kwenda kunichukulia chenji pale dukani?
2. B. Sawa, kwani uliacha shilingi ngapi?
3. A. Nilichukua soda tatu, nikampa elfu kumi (0.2) itakuwa elfu nane na mia mbili (0.2) ndio elfu nane na mia mbili.
4. B. Sawa. ((kisha akaondoka)).

Chanzo: Mazungumzo katika kibanda cha mamantilie, Dar es Salaam, (2022).

Katika data Na. 8 mzungumzaji A ameuliza swali “Hivi unaweza kwenda kunichukulia chenji pale dukani?”. Mzungumzaji B anajibu “sawa” badala ya “ndiyo” kwa maana ametambua kuwa mzungumzaji A anaomba msaada na si kutaka kujua uwezo wake wa kwenda kuchukua chenji. Ili kubaini kuwa hili ni swali la kawaida au “Swali la balagha” mtafiti alizingatia matendo-uneni athira. Kitendo cha mzungumzaji B kuitikia sawa kinaonesha wazi kuwa swali liloulizwa halihitaji majibu bali utekelezaji wa tendo-uneni kitovu ambalo ni ombi. Pia, utekelezaji wa ombi unaashiria kuwa kilachoelewka katika swali ni kuwa mzungumzaji A anamwomba mzungumzaji B akamchukulie chenji dukani. Makala hii imebaini kuwa kitenzi “weza” kinapotumiwa katika swali kinadhihirisha utu au lugha ya staha kwa wazungumzaji. Mfano; katika data Na. 8,

mzungumzaji amaetumia swali lililoundwa na kitenzi weza ili kuonesha utu.

Pia, katika utafiti huu imebainika kuwa swali linapotumia kitenzi “weza” katika ukanushi “huwezi”, basi swali hilo hubeba dhima ya amri. Hii ilidhihirika katika muktadha wa wazungumzaji kuwa na hadhi tofauti ambapo mwenye hadhi ya juu ndiye aliyebainika kuuliza swali husika kwa maana ya tendo-uneni la kuamrisha. Data ifuatayo inadhihirisha hili:

Data Na. 9:

1. A. ((Baada ya kuingia na kuona mmoja anafanya kazi mwagine amekaa bila kufanya kazi)) Hivi huwezi hata kumsaidia mwenzako? ((analiza huku akiwa amekunja uso)).
2. B. ((Anaamka na kwenda kumsaidia mwenzake)).

Chanzo: Mazungumzo katika kibanda cha mamantilie, Mbeya (2022).

Katika muktadha wa data Na. 9, mzungumzaji A ametumia kitezi “weza” katika ukanushi “huwezi” na kufanya swali lieleweke kama amri. Pamoja na matumizi ya kitenzi hicho katika ukanushi, kinachochocheara ubalagha ni uhusiano wa wazungumzaji pamoja na ishara za uso. Katika utafiti maswali yaliyoundwa na kitenzi “huwezi” na yaliyotokea mionganini mwa wazungumzaji wenye uhusiano wa hadhi tofauti hususani kicheo, yamedhihirika kuwa na dhima ya kuamrisha na si kuomba. Jambo hili halijazungumzwa na watafiti tangulizi kama Sadock (1971; 1974), Han (2002), na Sakamoto (2018).

Hata hivyo, kwa wazungumzaji wenye hadhi sawa swali lionaloambatana na kitenzi “huwezi” linawakilisha tendo-uneni la kulaumu au kukosoa badala ya amri. Data ifuatayo kutoka katika mazungumzo ya kwenye kibanda cha mamantilie inadhihirisha hili:

Data Na. 10:

1. A. Ah! Yaani, mkono wangu umechoka kweli, halafu wewe muda wote huo unaniangalia tu. Hivi huwezi kunibebea hata hiki?
2. B. Sasa mimi ningejuaje kuwa unahitaji msaada? Ha ha ha! Funguka! ((kisha anamsaidia)).

Chanzo: Mazungumzo katika kijiwe cha bodaboda, Mbeya (2022).

Katika data Na. 10, mzungumzaji A ametumia kitenzi “huwezi” kuunda swali lake. Matumizi ya neno hili katika swali husika yanafanya swali husika libebe dhima ya kulaumu au kukosoa kuliko swali kutaka kujua uwezo alionao mzungumzaji wa kubeba kitu husika. Katika muktadha wa mazungumzo haya, uhusiano wa wazungumzaji, yaani, uhusiano wa karibu umefanya swali husika lipate nguvu ya fasiri ya kibalagha. Wazungumzaji wanaonekana kuwa katika hadhi sawa na wana hali ya mazoea kama vile utani. Hili limedhihirishwa na majibu ya mzungumzaji B pale anapojitetea kuwa asingeweza kujua kama mzungumzaji A anahitaji msaada. Kujitetea kwa mzungumzaji B kunaashiria kuwa ombi la mzungumzaji A limeambatana na lawama.

5.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, Makala hii inaonesha kuwa katika mazungumzo ya Kiswahili, maswali ya balagha huweza kubainishwa kwa kuzingatia viashiria vya mofolojia. Kupitia Makala hii, vipashio vya kimofolojia vinavyoweza kuchochea fasiri ya kibalagha vimebainishwa. Makala hii inahitimisha kwa kusema kuwa ingawa kuna viashiria vya kimofolojia katika ubainishaji wa maswali ya balagha, muktadha wa matumizi una nafasi kubwa ya kuvifanya vipashio hivyo viwe na nguvu zaidi ya kuashiria ubalagha. Matokeo haya yanaelekeana na tafiti zingine zinazoonesha kuwa maswali ya balagha huweza kuashiria na vipashio vyote vya kiisimu na kimuktadha. Pamoja na kuelekeana huko katika matokeo, bado utafiti huu umeonesha namna vipashio vya kimofolojia vinavyotumika kuashiria maswali ya balagha katika mazungumzo ya Kiswahili. Hivyo, Makala hii imeongeza maarifa kuhusiana na ubainishaji wa maswali ya balagha kwa kudhihirisha baadhi ya vipashio vya kimofolojia vinavyoweza kubainisha maswali ya balagha katika mazungumzo ya Kiswahili. Mapendekezo ya Makala hii ni kuwa tafiti nydingine zinaweza kufanyika ili kuendelea kuibua maarifa kuhusiana na maswali ya balagha kama matendo-uneni yasiyorwazi katika lugha ya Kiswahili na lugha nydingine za Kibantu.

Jedwali la Alama za Unukuzi Zilizotumiwa katika Makala Hii

Unukuzi wa Alama kwa Mujibu wa Jefferson (2004)	
Alama	Maana
Namba za Tarakimu. Mfano; 1,2,3,4...	Majina ya wazungumzaji
A, B, C...	Zamu za kuzungumza
(0.2)	Pumziko la kuzungumza (namba huweza kuongezeka kulingana na muda wa pumziko)
(())	Maelezo ya mnukuzi kuhusu muktadha na viziadalugha
::	Urefushaji wa sauti (waka)
?	Kiimbo cha kuuliza
!	Kiimbo cha kushangaa
...	Kuna mazungumzo yameondolewa
↓	Kiimbo cha kushuka

MAREJELEO

- Athanasiadou, A. (1990). The Discourse Functions of Questions. A Revised Edition Paper Presented in 9th World Congress of Applied Linguistics, April 15-21. Halkidiki, Greece.
- Austin, J. L. (1962). *How to Do Things with Words*. Oxford: Oxford University Press.
- Bach, K. na Harnish, R. M. (1979). *Linguistics Communication and Speech Acts*. Cambridge: MIT Press.
- Bhattasali, S., Cytryn, J., Feldman, E., na Park, J. (2015). Automatic Identification of Rhetorical Questions. Makala iliyowasilishwa katika *Proceeding of the 53rd Annual Meeting of the Association for Computational Linguistics and The 7th International Joint Conference on Natural Language Processing*, Terehe 26-31, Julai 2015. 743-749. Beijing, China.
- Birner, B. T. (2013). *Introduction to Pragmatics*. UK: Wiley Blackwell.
- Dehé, N. na Braun, B. (2019). The Prosody of Rhetorical Questions in English. *Journal of English Language and Linguistics*, 1-29.
- Fiengo, R. (2007). Asking Question: Using Meaningful Structures to Imply Ignorance. New York: Oxford University Press.
- Frank, J. (1990). You Call That A Rhetorical Question? Form and Functions of Rhetorical Questions in Conversation. *Journal of Pragmatics*, 14: 723-738.
- Graham, K. (1977). *J. L. Austin: A Critique of Ordinary Language Philosophy*. London: Harvester.
- Han, C. (2002). Interpreting Interrogatives as Rhetorical Questions. *Lingua*, 112: 201-229.
- Ilgizovna, I. L. (2018). The Pragmatic Potential of Rhetorical Questions in English Informal Speech. *Eurasian Scientific Association*, 9: 43-55.
- Ilie, C. (1994). *What Else Can I Tell You?: A Pragmatic Study of English Rhetorical Questions as Discursive and Argumentative*. Stockholm: Almqvist and Wicksell International.
- Jefferson, G. (2004). Glossary of Transcript Symbols with an Introduction. Katika G. H. Lerner (Mh) *Conversation Analysis: Studies from the First Generation*. Amsterdam: John Benjamin Publishing Company. 13-31.
- Jeong, S. (2018). The Discourse Uses of the Korean Interrogative Sentence Enders -Na-(u), Nka, -Nya and -Ni. PhD Thesis. University of California.
- Kibiki, M. J. (2020). *Uchunguzi wa Vialami Pragmatiki katika Kiswahili cha Mazungumzo*. Tazmili ya Uzamivu (Haijachapwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Lakoff, R. (1973). Questionable Answers and Answerable Questions. Katika R. B. L. Braj, B. Kachru, Y. Malkiel, A. Pietrangel, S. Soporta (Wah), *Issues in Linguistics. Paper in Honor of Henry and Renee Kahane*. Urbana University of Illinois Press. 453-567.
- Sadock, J. M. (1971). Queclaratives. *Chicago Linguistic Society*, 7: 223-231.
- Sadock, J. M. (1974). *Some Covert Illocutionary Acts in English- Towards a Linguistic Theory of Speech Acts*. New York: Academic Press.
- Sakamoto, A. (2018). Rhetorical Questions Formations in Japanese and English. Katika Y. Ono na M. Shimada (Wah). Data Science in Collaboration, 1:155-164: General Affairs Supporting Center.
- Schmidt-Radefeldt, J. (1977). On So Called Rhetorical Questions. *Journal of Pragmatics*, 1: 357-392.
- Searle, J. R. (1969). *Speech Acts: An Essay in the Philosophy of Language*. London: Cambridge University Press.
- Searle, J. R. (1979). *Expression and Meaning: Studies in the Theory of Speech Acts*. New York:
- Wang, X. (2014). A Cognitive Pragmatic Study of Rhetorical Questions. *English Language and Literature Studies*, 4(1): 42-47.
- Wang, W. (2021). Pursuing Common Ground: Nondisaffiliative Rhetorical Questions in Mandarin Conversations. *Research on Language and Social Interaction*, 54(4): 355-373. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1080/08351813.2021.1974746>. Ilisomwa tarehe 7 Februari 2022.

Cite This Article: Sikitu Elias, Pendo Salu Malangwa, Dkt. Musa Mohamed Shembilu (2025). Ubainishaji wa Maswali ya Balagha kwa Kuzingatia Viashiria vya Kimofolojia katika Mazungumzo ya Kiswahili. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, 8(5), 131-138.
